**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**
**KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 20/10/2021.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1. Josephat Sangatati Mwenyekiti Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
2. Singisbert Themistocles Katibu Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
3. Constatine Mudende Mjumbe Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika
4. Reinfrida Anzigary Mjumbe Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria
5. Enock Ntakisigaye Mjumbe Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
6. Egidy Teulas Mjumbe Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi
7. Emmanuel Kulwa Mjumbe Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii

**SEKRETARIET**

1. Perpetua Lutwaza Sekretariet
2. Raymond Leonard Sekretariet
3. Godfrey Benedicto Sekretariet

**WAKARIBISHWA**

1. Jusline Bandiko Afisa Elimu Msingi
2. Simon Mtuka Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto
3. Costantino Msemwa Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji.

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 08/09/2021
4. Yatokanayo
5. Kujadili na kupitisha manunuzi ya Ujenzi na Ukamilishaji wa miundombinu ya majengo katika Shule za Msingi na Sekondari.
6. Kujadili na kupitisha taratibu za manunuzi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 39 katika Shule za Msingi Shikizi 6 na madarasa 77 katika Shule za Sekondari 23 zilizopokea fedha za UVIKO-19, Jengo la Dharura (EMD) na Nyumba ya Watumishi.
7. Kujadili na kupitisha manunuzi ya Halmashauri yasiyo ya Miradi ya Ujenzi.
8. Kufunga kikao.

**AGENDA NA. :- 19/2021/2022; KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 2.00 asubuhi akiwakaribisha wajumbe na kuwaeleza kuwa kikao hiki kimeitishwa ili kujadili hatua iliyofikiwa juu ya manunuzi yatakayofanyika moja kwa moja katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari baada ya kupokea fedha kutoka Hazina.

Katika maneno ya utangulizi wakati wa kufungua kikao Mwenyekiti alisema kuwa kikao kitajadili utaratibu wa manunuzi yatakayofanyika katika miradi iliyopokea fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Aliendelea kutaja kuwa kwa kuzingatia mwongozo wa utaratibu wa kuomba fedha kutoka Hazina kwa mpango wa bajeti wa mwaka 2021/2022 uliotolewa, Shule na Vituo vya kutolea huduma za Afya viliruhusiwa kuanza hatua za kutafuta mafundi na wazabuni wa kuuza vifaa vya viwandani na vifaa visivyo vya viwandani.

**AGENDA NA. :-20/2021/2022; KURIDHIA AGENDA.**
Wajumbe walikubaliana na agenda zote zilizowasilishwa ili zijadiliwe.

**AGENDA NA. :-24/2021/2022; KUJADILI NA KUPITISHA TARATIBU ZA MANUNUZI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 39 KATIKA SHULE ZA MSINGI SHIKIZI 6, MADARASA 77 KATIKA SHULE ZA SEKONDARI 23, UJENZI WA JENGO LA DHARURA (EMD) NA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUMISHI KWA FEDHA ZA UVIKO-19**

Katika agenda hii wajumbe walipokea barua zilizotoka Idara ya Elimu Msingi, Idara ya Elimu Sekondari na Idara ya Afya kwa ajili ya kuomba idhini ya Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kuanza manunuzi kwa kutumia fedha za UVIKO-19.

Wakijadili kuhusu taratibu za manunuzi ya miradi hii, kikao kilianza kwa kupitisha njia ya manunuzi ya "Force Account" kwa ujenzi wa madarasa ya Shule za Sekondari na madarasa ya Shule Shikizi za msingi ambazo zimetengewa jumla ya Tsh.2,320,000,000/=.

- Ili kuhakikisha kazi zinakamilika kwa wakati, wajumbe wa kikao walikubalia kuwa kwa vifaa vya viwandani yafanyike manunuzi ya pamoja "Bulk Purchase" kutoka moja kwa moja viwandani au kwa mawakala wa viwanda.
- Kutumia jeshi la magereza kwa ajili ya upatikanaji wa kokoto ambapo Gereza la Rusumo linazalisha kokoto kwa kutumia "crusher".
- Kutumia njia za ushindanishaji "Competitive Quotation" kwa ajili ya kupata mafundi "local fundi" wa kujenga madarasa.
- Vifaa vya ujenzi visivyo vya viwandani kama vile mawe, mchanga, kokoto, mbao na tofali kununuliwa moja kwa moja kwa wazabuni wenye mikataba ya GPSA au kununua kwa wazalishaji wa vifaa hivyo na kuandaa taratibu za usafirishaji hadi maeneo ya miradi.

Wajumbe walipokea mapendekezo ya njia ya "National Competitive Bidding" ambapo waliruhusu njia hii itumike kwa miradi ya miwili ambayo ni Ujenzi wa Jengo la Huduma za Dharura (EMD) lililotengewa fedha kiasi cha Tsh.300,000,0000/= na Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi (3 in 1) itakayojengwa katika Zahanati ya Mumuhamba baada ya kutengewa fedha kiasi cha Tsh.90,000,0000/=. Kikao kiliagiza kuwa miradi hii miwili ya EMD na nyumba ya watumishi itangazwe kwa kupitia mfumo wa manunuzi wa TANePS ili kuongeza ushindani.

Kabla ya kuhitimisha agenda hii wajumbe wa kikao waliagiza kuwa kiitishwe kikao kitakachohusisha Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule ili kukumbushana taratibu za manunuzi na kuelekeza namna bora ya utekelezaji wa ujenzi wa madarasa yote 116 hadi kukamilika kwa njia ya "Force Account". Baada ya majadiliano na makubaliano hayo, Mwenyekiti aliruhusu agenda inayofuata kuanza kujadiliwa.

**AGENDA NA. 25/2021/2022; KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuitikia mwaliko wa kikao hiki muhimu kwa ajili ya kuandaa miradi inayotarajiwa. Aliwakumbusha wajumbe kuwa kikao kama hiki kilifanyika katika mwaka wa fedha uliopita na kisha fedha zikatolewa kwa mantiki hiyo Halmashauri itarajie kupokea fedha za miradi yote iliyojadiliwa ambapo tutapaswa kusimamia utekelezaji ili kufikia malengo tarajiwa. Alitamka kufunga kikao mnamo saa 4. 36 asubuhi.

**UMETHIBITISHWA:**

.............................
SingisbertThemistocles

**KATIBU**

.............................
Josephat Sangatati

**MWENYEKITI**

**TAREHE:** ...12/11/2021...